JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE.

SHULE YA SEKONDARI MNYUZI,
S.L.P 314 KOROGWE-TANGA,
SIMU: 0739998880; 0768866266. MKUU WA SHULE, 0678184496; MAKAMU MKUU WA SHULE, 0674976023; MWALIMU WA FEDHA
Email: mnyuzisec06@gmail.com

Kumb. Na. MNYZ/JOI/2022/02. **02.02.2022.**

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ……

S.L.P……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MNYUZI HALMASHAURI YA WILAYA KOROGWE, MKOA WA TANGA MWAKA 2022 KIDATO CHA TANO (5).

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano (V) Masomo/Tahasusi ya **History, Geography na English Language (HGL), na History, Kiswahili na English Language (HKL),** katika shule hii mwaka 2022,

Shule ya sekondari ya MNYUZI ipo umbali wa kilometa 22 kutoka kituo cha mabasi cha Wilaya ya Korogwe. Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi cha mji wa korogwe kuanzia asubuhi hadi saa 12:00 jioni nauli ni shilingi **3,000 Bajaji**. Shuka Mnyuzi. Chukua Bodaboda/Pikipiki Nauli **1,000/=** ikupeleke shule ya sekondari ya ***MNYUZI (kwa wanaotoka njia ya Arusha Dar es salaam nakushuka stendi Korogwe), Kwa wanaotoka Tanga shuka Maguzoni kisha chukua pikipiki nauli 2000.***

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **04 JULY 2022.** unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe **04 JULY 2022.** Na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22 Julai 2022. (**Pia zingatia maelekezo yatakayotolewa na wizara)**
NB. MZAZI/MLEZI Mwandalie mapema mwanao mahitaji yake mapema na aripoti mapema maana masomo yataanza wiki ya kwanza siku ya pili.

Mambo ya kuzingatia

1. ADA NA MICHANGO YA SHULE.

a. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=, Unaweza kulipa TSh.35, 000/= kwa muhula.

b. Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. Shilingi 15,000/= Ukarabati wa samani.

ii. Shilingi 6,000/= Kitambulisho na picha.

iii. Shilingi 20,000/= Taaluma.

iv. Shilingi 30,000/= Kuwalipa wapishi walinzi na vibarua wengine.

v. Shilingi 2,000/= Nembo 1 ya shule.

vi. Shilingi 10,000/= Kwa ajili ya huduma ya kwanza.(Haitarejeshwa)

vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima (Mock)

viii. Fedha ya tahadhari 5,000/= (Haitarejeshwa).

Fedha hizoza **ADA na Michango** jumla yake kwa **mwaka ni 178,000/= ZITALIPWA KWA CONTROL NUMBER,** HIVYO PIGA SIMU KWA MKUU WASHULE AU MWALIMU WA FEDHA ILI AKUPE CONTROL NAMBA**. KAMWE USITUME FEDHA KWA MWALIMU, LIPA KWA NJIA YA BENKI, WAKALA WA BENKI, AU WAKALA WA SIMU UNAYEMFAHAMU.**
MKUU WA SHULE= 0739998880; 0768866266, 0658600066. MWALIMU WA FEDHA=0674976023;

2. Sare za Shule

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vitu vifuatavyo kwa ajili ya sare za shule:-

Sare za shule zitashonwa kwa usimamizi shuleni na gharama ni kama ifuatavyo:

i. Sketi mbili- kijani Sh. 44,000/=)

ii. Sweta Sh.15,000/= Sweta rangi ya Zambarau mikono mirefu, iwe na V shingoni au nunua uje nayo

iii. T. Shirt moja Sh.12,000/= (Ukitaka mbili lipa sh.24000/=) zitapatikana shuleni kwa utaratibu maalum.

iv. Hijabu rangi nyeupe (tetron) Kwa mwanafunzi Mwisilamu.Hijabu **iwe nyeupe isiyo na urembo wa aina yoyote au kufungwa na urembo wowote HIJABU IWE NDEFU IFUNIKE MIKONO AKISHUSHA CHINI.**

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba, viwe na visigino vifupi.

vi. Soksi nyeupe jozi mbili za shule.

vii. Nguo za kazi na kushindia eneo la shule (shamba dress), (gauni mbili mikono mifupi rangi ya damu ya mzee liwe refu ukisimama iwe na lisibane mwili) NGUO ZOZOTE ZA NYUMBANI USIJE NAZO S**H**ULENI hutaruhusiwa kuvaa shuleni.

viii. Mashati mawili (2) meupe. Mikono mirefu {NJOO NAYO}. – unaweza pia kushona hijabu rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule ambayo ni nyeupe.

ix. Suruali Kwa Wasichana Hairuhusiwi Kabisa.

N.B. Fedha za mashono zitalipwa taslimu shuleni siyo njia ya Benki.

Mshono Wa Sketi Au Gauni ni Rinda Box 4, Sketi Iwe Ndefu Iguse Kiwiko/Kifundo Cha Mguu Kwa Wanafunzi Wote, Usishone Kwa Mazoea, Fuata Maelekezo Tuliyotoa (**sketi au gauni fupi isiyozingatia maelekezo haitakubalika na hutaruhusiwa kutumia shuleni**).

3. Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo;

(i). T-sheti nyekundu isiyo na picha, mchoro wala maandishi

(ii). Bukta rangi ya Blue.

(iii). Sketi ya rangi ya Orange ya kuzunguka kwenye bukta

(iv). Raba nyeupe au nyeusi, raba ziwe za kufunga na kamba.

(v) Track suit rangi ya blue (Dark Blue) itatumikapia kwa **kushindia**, **kusomea usiku na michezo**.

4. Mahitaji ya taaluma shuleni.

A. Uje na **Rimu 2 (mbili) A4 (PLAIN/Isiyo na mistari),** moja kwa kila muhula (itatumika kuzalishia mitihani na matumizi mengine ya ofisi na siyo ya kufanyia mitihani) nunua madaftari na karatasi za kufanyia mitihani shuleni (Rimu(ruled) binafsi ya mwanafunzi karatasi za mistari ni nzuri zaidi .

B. Madaftali makubwa 12, kalamu za kutosha ma mathematical set moja. **NB. Nunua Madaftari Kabla Ya Kitu Kingine Chochote.**

C. Vitabu vya dini na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi.

D. Nunua Vitabu vya masomo yako kadiri ya tahasusi yako uliyochaguliwa.

F. Files 3 kwa ajili shule na mwanafunzi shuleni.

<u>Mwanafunzi pia aje na vitu vifuatavyo pindi anaporipoti shuleni.</u>

5. Huduma ya afya na Vifaa vya Usafi vya shule

HGK	**Hard bloom 1, Jembe lenye mpini 1, Kwanja 1, Ndoo kubwa 1.**
HKL	**Squeezer 1, Toilet Blush 1, Kwanja 1,** Soft bloom 1, **Ndoo kubwa 1.**

Utalipia Tshs 5,000/= bima ya afya. (Kama una Bima ya Afya **NHIF hutalipa 5000).**

6. Mahitaji Mengine ya mwanafunzi.

(i) Ndoo, sahani (Bati), kijiko na kikombe (Bati). Vyombo vya Plastiki havitakiwi shuleni.

(iv) Shuka mbili za rangi pink na blanketi moja (andika jina lako pembezoni mwa shuka)

(vi) Taulo, malapa, mswaki, kanga/vitenge viwili,mto, nguo ya kulalia ambayo huruhusiwi kutoka nayo nje ya bweni na mahitaji mengine muhimu ya mtoto wa kike.

(vii) Tochi ndogo dharura za usiku.

(viii) Chandarua kimoja rangi nyeupe.

(ix) Njoo na Godoro ich 4 ya futi 3/6.

7. **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

1) Wizi**.**
2) **.** Uasherati na ushoga.
3) Ubakaji
4) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, kama vile uvutaji wa bangi cocaine, mirungi, kuberi, sigara, .n.k.
5) Kupiga au kupigana. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
6) Kudharau bendera ya taifa.
7) Kuoa au kuolewa.
8) Kugoma au kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
9) Kukataa adhabu kwa makusudi.
10) Kutotimiza kwa makini maandalio ya jioni (prep.) na siku za mwisho wa wiki.
11) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na **simu** ya mkononi, redio, na pasi ya umeme, au kifaa chochote kinachotumia umeme, Ukikutwa na simu ya mkononi, "line/chip" Ya simu au "smart watch" yenye uwezo wa simu mahali popote ndani ya eneo la shule au nje ya shule kwa muda/siku za masomo utafukuzwa au kusimamishwa shule wakati huohuo, simu na line itakayokamatwa shuleni itahesabika kama kusudio la kuleta madhara katika rasilimali zingine za shule, ukikamatwa na simu bila madhara mengine simu hiyo kabidhi bila vurugu na hutarudishiwa, na utalipa ***faini Tsh.50,000/=*** , kama simu italeta madhara utalazimika kulipa gharama ya hasara uliyosababisha pamoja na faini tajwa
12) **Unaruhusiwa kusafiri na simu kwa mawasiliano ya njiani**, ukifika shuleni basi ikabidhi kwa uongozi wa shule mara moja, kamwe ukiingia shule usiingie nayo darasani wala bwenini,wala kuzunguka nayo shuleni, kabidhi ufikapo shule na **siku ya kufunga shule utakabidhiwa simu yako salam**a. Ukishakabidhi simu hutaruhusiwa kuitumia mpaka siku ya kufunga shule hivyo usimsumbue mwalimu kwa

kuidai au kuomba kwa matumizi yoyote, nakili namba za simu za wazazi/walezi wako sehemu nyingine ukihitaji mawasiliano au matumizi tumia utaratibu ulioelekezwa.

13) Kwa mawasiliano na wazazi mwanafunzi atumie simu ya Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule, Mwalimu wa fedha, Mwalimu wa malezi (Nidhamu), Mwalimu wa nyumba (matron), mwafunzi haruhusiwi kutumia simu ya mtu mwingine nje na waliotajwa, ikitokea mwanafunzi ametumia simu ya mtu asiye mwalimu nje au ndani ya shule atafukuzwa shule au kusimamishwa shule au adhabu kali.

14) Hakutakuwa na ruhusa ya kuzurura (outing) nje ya shule katika siku za masomo (uwapo shuleni), ILA kunaweza kukawa na **ZIARA Rasm**i za wanafunzi zitakazogharimiwa na wazazi kwa lengo la mafunzo nje ya shule zenye ruhusa rasmi za mamlaka zinazohusika.

15) Siku za ibada muda wa ibada ukiisha wahi shule bila kuzurura mtaani au kwenda katika nyuma za watu wengine ikiwemo walimu ni kosa.

8. **Sheria na kanuni muhimu za shule**

3.1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria namba 26 ya mwaka 1970. Aidha inazingatia miongozo yote ya Wizara yenye dhamana ya elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi;

(A), Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima**.**

(B), Mahudhurio mazuri kwa kila KIPINDI NA shughuli nyingine ndani na nje ya shule ni LAZIMA.

(C). Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.

(D). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii, Huruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum (maandishi) kwa mwalimu au kiongozi mwenye dhamana.

(E). Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(F). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa**.**

(G) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(H). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa.

(I). Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amenyoa nywele robo chini

(J) Wasichana hawaruhusiwi kusuka au kufuga nywele ndefu.

(K) Kwa mwanafunzi ambaye atasababisha mikusanyiko isiyo rasmi na isiyo na kibali au kuchochea vurugu, migomo au utovu wa nidhamu atasimamishwa na kuachishwa shule.

9. **Mambo mengine muhimu.**

A), Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(B). Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

(C). Fomu ya mzazi au mlezi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni , na maelezo mengine yatolewayo na shule.

Tafadhali soma maelekezo haya kwa makini na kuyatekeleze kikamilifu

KWA JAMBO LOLOTE USILOELEWA VIZURI WASILIANA NA MKUU WA SHULE AU MAKAMU MKUU WA SHULE. KWA NAMBA HIZI. **0739998880, 0768866266, MKUU WA SHULE na 0678184496 MAKAMU MKUU WA SHULE,**

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA MNYUZI.

SULLE, WILLIAM .N.

HEADMASTER
MNYUZI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX
KOROGWE

MKUU WA SHULE.

OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V).

SHULE YA SEKONDARI MNYUZI

(B). REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

MNYUZI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 314,
KOROGWE.
DATE 12.12.2022.

MEDICAL OFFICER,

……GOVERNMENT HOSPITAL/ H.C. (Jina la Hospitali ya serikali).

NAME OF STUDENT: ……

Please examine the above named student to ascertain his/her fitness for further studies.

……**HEAD OF SCHOOL.**

MEDICAL CERTIFICATE:

[To be completed by the medical officer].
I have examined the above named students with regard to:
Skin …… Eyes ,……
Ear……Chest……..……Eyes …… Spleen ……
Abdomen …… Urine ……..Stool ……
Hemoglobin …… Sickle …… cell ……
others……
And I considered.

1.He/She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzia, and fit to go to school.

2. He/She is now to return to school having treatment ……

Name……..…….. & signature……. of medical officer

Date: ……

NB. <u>FOMU HII IWE IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI UTALETA SHULE SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti) MWANAO SHULENI IKIWA IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI TAYARI NA IGONGWE MUHURI WA HOSPITALI HUSIKA.</u>

OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V).
SHULE YA SEKONDARI MNYUZI

SHULE YA SEKONDARI MNYUZI,

S.L.P 314,

KOROGWE.

TAREHE 12.12.2022

(C). FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA.
SEHEMU A; **Taarifa za mwanafunzi.**

1.Jina kamili (mwanafunzi)……

2. Tarehe ya kuzaliwa (mwanafunzi) …….

3. Wilaya alipozaliwa (mwanafunzi) …… kata …….. kijiji……..……

4. Kukubali nafasi**. (Ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi (Jina la mwanafunzi) ……..……. nimesoma na kuelewa maagizo yote ya shule ya sekondari ya Mnyuzi na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Mnyuzi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya mwanafunzi ……. Tarehe …….

SEHEMU B; Taarifa za **mzazi/mlezi**(**Ijazwe na mzazi /mlezi**).

1. Jina kamili la mzazi/mlezi……..……
2. Mimi ni mzazi/mlezi? ……..…….
3. Kazi yako …….
4. Anwani ya mzazi/mlezi. …….
5. Namba tatu za simu ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi

(a)……..……(b)……(c)……..……

UTHIBITISHO

Mimi.mzazi/mlezi wa ……..……..

Nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu **sehemu A hapo juu.**

Sahihi ya mzazi/mlezi…….. Tarehe……
Taja Majina na simu za ndugu wengine au mzazi anayeweza kumtembelea mwanafunzi shuleni na inapotokea tatizo.
1.Jina ……..simu……., ……..
2.Jina ……simu ……., ……
3.Jina ……..simu ……..,……

NB. <u>FOMU HII IWE IMEJAZWA NYUMBANI NA MZAZI PAMOJA NA MWANAO, UTAIKABIDHI FOMU HII SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti) MWANAO SHULENI IKIWA IMEJAZWA TAARIFA ZOTE MUHIMU.</u>

NJOO NA VITABU VYA COMBINATION YAKO MUHIMU SANA.

HISTORY -

- Major events in the world History by Gervas
- Kato, A (2011) Mastering Advanced Learners History for Form 5&6
- Oxford (2011) Advanced Learners History Form 5 & 6 Zombwe

GEOGRAPHY -

(a) Contemporary issue in Geography by Msabila

(b) (b) Integrated approach Geography

© Essential of practical Geography Advanced level (Form 5 & 6)

- Zist, K (2015) ,Geography Paper Two, Human and Economic Geography
- Zist, K (2016), Physical Geography Paper One

KISWAHILI – Riwaya: Vuta ni kuvute, Usiku utakapokwisha,Mfadhili na Barua ndefu kama hii.

Ushairi: Kimbunga, Na Chungu Tamu. **Tamthilia:** Nguzo mama, Kwenye ukingo wa thim, Morani

- Oxford University Press (2012) Kiswahili Kidato cha Tano na Sita
- Nyangwine Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 Kidato cha 5 na 6
- J .A. Masebo (2006) Nadharia ya Fasihi Kiswahili 2 Kidato cha 5 na Sita
- Tahakiki vitabu teule vya Fasihi kidato cha Tano na Sita J. A Masebo&Nyambari Nyangwine 2008

DICTIONARY – Kiswahili ya TUKI

GENERAL STUDIES -

- Mwajabu, M (2016) Comprehensive Book for Advanced Level Secondary School
- Nyambari, N & Bukagile, R (2010), Contemporary Approach for Advanced Level General Studies Form 5 & 6

REVIEWS – HISTORY 1 & 2, GEOGRAPHY 1& 2, KISWAHILI 1&2, GENERAL STUDIES

ENGLISH:

- English Paper One. Ashel, N (2010): Advanced Level English a practical Approach
- Paper Two. Ashel N (2011) Advanced Level Literature An Essential Guide
- Nyambari Nyangwine (2008): Advanced Level Literature

NB.

- ***VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI, WALAU KITABU KIMOJA KWA SOMO***
- ***KWA MZAZI ANAYEPENDA MWANAYE AFAULU KWA VIWANGO VYA JUU MNUNULIE MWANAO VITABU MUHIMU.***